

MSIFUNI BWANA HUWAPONYA WALIOPONDEKA MOYO

Yohana J. Magangali
NM-AIST, Arusha

M si fu ni Bwa na msi fu ni Bwa na

Hu wa po nya wa li o po nde ka mo yo mo yo

MASHAIRI YASOMWE

1. Ee nafsi yangu umsifu Bwana,
nitamsifu Bwana maisha yangu yote;
nitamwambia Mungu wangu ningali hai
2. Usiweke tumaini lako kwa wakuu,
kwa wanadamu ambao hufa,
ambao hawawezi kuokoa;
roho zao hrudi mavumbini,
mipango yao siku hiyo hukoma.
3. Heri yeye ambaye,
Mungu wa Yakobo ni msaada wake;
ambaye tumaini lake ni Bwana Mungu wake,
muumba wa mbingu na dunia,
bahari na vyote vilivyomo;
ni mwaminifu milele na milele.
4. Bwana ni mwenye haki,
katika njia zake zote,
na mwenye upendo,
kwa vitu vyote alivyovifanya;
Bwana yu karibu kwa wote wamwitao,
wamwitao kwa uaminifu.